Ukweli wa mambo – Habari ya Jumla

(yapatikana katika lugha zenginezo)

Kansa ya matiti ni nini?

Kansa ya matiti ni kusanyiko la seli zisio za kawaida zinazoendelea kukua na kuongezeka kwa idadi. Mwishowe hizi seli huenda zikaumba bonge kwenye titi. Kama kansa haikutolewa au kuzuiliwa seli za kansa zinaweza kuenea kwenye viungo vingine via mwili na mwishowe inaweza kusababisha kifo.

Jee niko hatarini ya kutambuliwa na ugonjwa wa kansa ya matiti kupitia dalili zilizopo?

Mmoja kati ya wanawake wanane wa-Australia watakua na kansa ya matiti maishani mwao.
Hatari muhimu zaidi ya kusababisha kansa ya matiti ni kuwa mwanamke wa miaka hamsini na kuendelea.

Jee kinga kupitia uchunguzi wa matiti ni nini?

Kinga kupitia uchunguzi wa matiti ni eksrei ya kipimo cha chini zaidi ya titi la mwanamke ambaye kwa namna nyengine yoyote hana badiliko au jambo lisilo la kawaida kwenye titi lake. Kinga kupitia uchunguzi wa titi hugundua asilimia tisini za kansa ya matiti na inaweza kuonyesha kansa ya matiti ambayo ni ndogo sana kutambulika kwa kugusa. **Ugunduaji mapema ndio kinga yako bora zaidi.** Kuipata kansa hapo mwanzoni inaongezea fursa ya matibabu kufaulu.

Nina hitaji kwenda kuchunguzwa mara ngapi?

Kwa desturi kila baada ya miaka miwili uchunguzi wa matiti unashauriwa kwa wanawake wa umri wa miaka hamsini na kuendelea. Walakini, kuna nyakati uchunguzi wa matiti unashauriwa kufanyika kila mwaka.

Jee kinga kupitia uchunguzi wa matiti ni bure?

BreastScreen WA inasaidiwa kwa malipo na serikali ili ipeana huduma ya uchunguzi wa matiti **BURE** kila baada ya miaka miwili kwa wanawake wa miaka hamsini hadi sitini na tisa. Wanawake wenye umri arobaini hadi arobaini na tisa na pia zaidi ya miaka sabini wanaweza kufanyiwa uchunguzi wa matiti wa bure na BreastScreen WA wakiomba. Huduma ya uchunguzi wa matiti **HAIPATIKANI** kule BreastScreen WA kwa wanawake walio chini ya miaka arobaini.

Jee ninaweza kufanyiwa huu uchunguzi wa matiti wapi?

BreastScreen WA ina vituo saba vya huduma mjini katika sehemu ya Cannington, Fremantle, Joondalup, Midland, Mirrabooka, Perth mjini na Rockingham na vituo vine vya kusafarishwa na gari ambavyo huhudumia walioko mashambani kila baada ya miaka miwili.

Jee nini hutokea ninapo tembelea BreastScreen WA?

Ukikuja kuhudumiwa mle BreastScreen WA unashauriwa **uvae nguo ya juu na ya chini,kwa mfano sketi au suruali na shati na pia unashauriwa kutopaka poda au kutumia dawa ya kuondoa harufu mbaya.**
Unapofika BreastScreen WA utaratibu huu utafuatiwa:

1. Utakaribishwa na kuulizwa ujaze fomu za habari yako binafsi na pia ya kupeana idhini yako.
2. Ukishavaa ile gauni, mpiga picha za eksrei wa kike atakuingiza kwenye chumba cha eksrei na kukuuliza maswali machache. Kisha atachukua picha mbili za eksrei za kila titi.
3. Utaombwa kusubiri mpaka mpigaji hizo picha azitizame eksrei kuhakikisha hazina hitilafu ya kiufundi yoyote.
4. Mpiga picha za eksrei atakujulisha wakati uchunguzi umekamilika na unaweza kuondoka.
5. Eksrei zako zitakaguliwa upya na madaktari wasiopungua wawili ambao wanaujuzi spesheli na utatumiwa matokeo kabla ya siku kumi na nne za kazi kupita.
6. Sio jambo lisilo la kawaida kwa wanawake kuitwa wafanyiwe eksrei zaidi tena. Kama hii ikihitajika muuguzi au nesi wa Uchunguzi wa Matiti kutoka BreastScreen WA atakuita kwa simu kuzungumzia hayo zaidi.

Uchunguzi wa matiti unafanyika vipi?

Titi linawekelewa kwa uangalifu kwenye mashine ya eksrei na kufinya kwa sekunde chache wakati eksrei ina chukuliwa. Eksrei mbili zinachukuliwa kila titi, moja kutoka juu na nyengine kutoka kwa upande. Kufinyilia kunaweza kubana na pia kupunguza starehe lakini hufai kuleta maumivu, lakini kufinyilia ni muhimu ile picha safi na bora zaidi ipatikane (tizame mfano ulioko mkono wa kulia hapa chini) na pia mnunurisho wa kipimo cha chini zaidi hutumiwa.





Bila kufinyilia eksrei yako haitaonekana dhahiri



Kwa kufinyilia eksrei yako inakua dhahiri zaidi

Mbona niende kufanyiwa uchunguzi wa matiti?

Ugunduaji wa mapema ndio kinga bora zaidi yako. Kinga kupitia uchunguzi wa matiti utaoko maisha yako.

Ahadi inaweza kupatikana kwa kupiga simu nambari moja tatu mbili sifuri tano sifuri(13 20 50).

Ukihitaji mkalimani wa bure, tafadhali pigia simu shirika la Kutafsiria na Ukalimani yaani Translating and Interpreting Service (TIS) kwanza kwenye simu nambari moja tatu moja nne tano sifuri (13 14 50), na kuomba kuunganishwa na ofisi kuu ya kuagiza huduma za BreastScreen WA katika nambari moja tatu mbili sifuri tano sifuri (13 20 50).

Ahadi za Vikundi

Ahadi za Vikundi zinapatikana kwa wanawake ambao wanapendelea kuenda pamoja kama kundi. Kwa mfano wanawake ambao wanazungumza lugha moja, wanawake ambao wako katika chama au shirika au marafiki wanaweza kufurahia kupanga kwenda pamoja kama kundi. Kwa maswali zaidi kuhusu ahadi za vikundi tafadhali piga simu nambari moja tatu mbili sifuri tano sifuri (13 20 50).

Vifaa vya bure

Kuna vitabu vidogo vya bure vya habari ambavyo unaweza kupata kuhusu kinga kupitia uchunguzi wa matiti, kansa ya matiti, wanawake wenye historia za jamii ambazo zimepatwa na kansa ya matiti, pandikizo, maumivu ya matiti, wanawake walio na ulemavu na mengineo.

Vifaa vinavyopatikana katika lugha zingine

'For Me and My Family' (video) ['Mimi na Jamii Yangu'] (kanda) inapatikana kwa lugha ya Kiarabu, Kicantoni, Kicroatia, Kiingereza, Kigriki, Kiitaliano, KiKhmer, Kimacedonia, Kirassia, Kipolandi, Kiserbia, Kispaniola, Kitagalog, Kituruki na Kivietnami.

Hii 'General Information – Fact Sheet' ['Habari ya Jumla – Ukweli wa Mambo'] inapatikana kwa lugha ya Kiingereza, Kiamharic, Kiarabu, Kibosnia, Kiburma, Kichina, Kicroatia, Kidari, Kifarsi, Kigriki, Kiindonesia, Kiitaliano, Kimacedonia, Kimalay, Kimalta, Kiholandi, Kikhmer, Kikorea, Kipolandi, Kiportugal, Kiserbia. Kisomali, Kispaniola Kiswahili, Kitagalog, Kithai, Kitigrigna na Kivietnami.

Ile 'After your screening mammogram – What next?' Fact Sheet ['Baada ya Uchunguzi wa matiti – Nini Inafuatia?'] Ukweli wa Mambo inapatikana kwa Kiingereza, Kiarabu, Kibosnia, Kichina, Kicroatia, Kidari, Kigriki, Kiindonesia, Kiitaliano, Kimacedonia, Kimalay, Kipolandi, Kiportugal, Kiserbia, Kispaniola na Kivietnami.

'Screening Mammography for Women with a Family History of Breast Cancer' ['Kinga Kupitia Uchunguzi wa Matiti Kwa Wanawake walio na Historia Ya Jamii ambazo Zimepatwa na Kansa Ya Matiti'] hupatikana kwa Kiingereza, Kibosnia, Kichina, Kidari, Kimalay, Kiserbia na Kivietnami.

Ukitaka kuagiza vifaa, tafadhali piga simu nambari tisa tatu mbili tatu sita saba sita mbili (9323 6762) au andika barua ya elektroniki kwa breastscreenwa@health.wa.gov.au